

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

Supplement No. 15

28th April, 2023

SUBSIDIARY LEGISLATION

To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 15 Vol. 104 Dated 28th April, 2023
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 304 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

AMRI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA IFUNDA YA MWAKA
2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Ifunda ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji la mpango wa urasimishaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mipangokina ya eneo

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

—
JEDWALI
—

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira – nukta773016MS, 9110827KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira – nukta773361MS, 9110315KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.9 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira – nukta 773269MS, 9109435KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 1.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P4 yenyemajira – nukta772849MS, 9108384KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 1.16 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P5 yenye majira – nukta 772126MS, 9107479KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 3.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P6 yenye majira - nukta769399, 9105084; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.58 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P7 yenye majira – nukta 768812MS, 9105065KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 1.28 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P8 yenye majira–nukta768068MS, 9105966KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P9 yenye majira - nukta768626MS, 9106267KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P10 yenye majira – nukta 768861MS, 9106826KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 2.0 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P11 yenye majira – nukta 768861MS, 9106826KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 5.5 hadi ulipoanzia”

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
Waziri wa Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi